



Kuliishi mfalme katika
Kisiwa cha Rusinga. Mfalme
huyo hakuwa amehisi
maumivu maishani mwake.

Hakuwahi hata dakika moja.



Asubuhi moja mfalme alikiinamisha kichwa chake. Aliwaza namna maumivu yanavyokuwa. "Kuna watu wengi maskini katika ufalme wangu. Nitawezaje kuhisi maumivu yao?" alijiuliza.




Mchana na usiku, alitamani
kuhisi maumivu angalu
mara moja tu.

Usiku mmoja, aliota ndoto
akasikia sauti ikisema,
“Nimesikia matakwa yako.
Utahisi maumivu.”




Sauti hiyo iliendelea,
“Yajenge mashua kubwa
saba ambamo utaweka mali
na familia yako. Kisha safiri
ukielekea upande wa
kaskazini mwa Kisiwa cha
Rusinga.”


Mfalme alifurahi sana.



Muda mfupi baadaye,
mashua saba yalijengwa na
wakawa tayari kusafiri.



Siku moja kabla ya safari,
mfalme aliandaa sherehe.
Kila mmoja alihudhuria.
Chui, nyoka, sungura,
konokono, ndege na hata
siafu, wote walifika kwa
sherehe.



Mfalme aliwahotubia watu,
“Mimi na familia yangu
tunaondoka kwenda
sehemu tofauti ya Kisiwa
cha Rusinga. Tunataka
kuhisi maumivu ambayo
watu wengine huhisi.”



Watu walinong'onezana
miongan mwao. Wazee
hawakumwamini.

Lakini, ni nani angemhoji
mfalme?



Siku iliyofuata, mfalme na familia yake walisafiri.

Kwa siku mbili, mashua yalipita majini. Anga lilikuwa wazi, bahari ilitulia na safari ilifurahisha.




Lakini siku ya tatu, bahari
ilichafuka. Anga libadilika
likatanda mawingu.
Walikumbwa na dhoruba
kubwa.

Mashua yalizama. Mfalme
hakuweza kufanya lolote.
Familia na mali yake
ilipotelea baharini.



Mfalme pekee alinusurika.
Lakini, alikuwa amebadilika
na kuwa mduria.

Mdiria aliruka akatua
ukingoni mwa bahari.
Alikuwa bado akitumaini
kuipata familia na mali yake
kutoka baharini.



Mdiria alipiga mbizi baharini mara nyingi. Hakuweza kuiokoa familia yake au hata baadhi ya mali yake.

“Kama ningejua,
ningeyafurahia maisha
yangu yalivyokuwa,” alilia.